# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**MOI GIRLS ELDORET**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# MOI GIRLS ELDORET KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**

**Karatasi ya 2**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**UFAHAMU**

(a) Changamoto za Ugatuzi/Matatatizo ya ugatuzi/Ugatuzi **( alama 1x1=01)**

(b)

- Ugatuzi ni mfumo geni. **(Alama 3x1=03)**
- Serikali kuu kutowajibika
- Kudai kuwa mfumo huu unahitaji mda zaidi

(c)

- Mfumo wa ugatuzi nchini umehusishwa matendo ya kibepari kama vile; **(alama 3x1=03)**
- Raia kupewa mzigo wa kulipa ushuru ili kuipa serikali mapato
- ushuru ndio njia kubwa ya kuzalisha mapato ya serikali zinazojifunga na mfumo wa kimagharibi wa kiuchumi
- viongozi kuwanyoya raia walio maskini

(d)

- Hali mbaya ya muundo msingi **(alama 4x1=04)**
- Viongozi kuendeleza ufisadi
- Ukosefu wa usawa katika ugavi wa rasilimali
- Viongozi kupuuza mchango wa wananchi

(e)

- Raia kulazimishwa kulipa ili kuona maiti za jamaa zao katika fuo **(alama 2x1=02)**
- Raia kurundikiziwa mzigo wa kulipa ushuru mkubwa
- Ushuru unaolipwa na wananchi hauwasaidii wananchi ila huishia mifukoni mwa viongozi

(f) (i) Ugavi wa mamlaka na rasilimali kutoka serikali kuu hadi mashinani **(alama 2x1=02)**
(ii)mfumo wa kiuchumi wa watu wachache kumiliki rasilimali kwa kuwapora wengine

***Ondoa nusu alama kwa kila kosa la sarufi hadi makosa sita.***

***Ondoa nusu alama kwa kila kosa la tahajia hadi makosa sita.***

**UFUPISHO**

**(a)**

- Nchi zinazoendelea huwa na masoko finyu
- Viwanda vikubwa hupata ugumu kufanya biashara katika masoko finyu
- Viwanda vidogo vinaweza kuwaajiri wafanyakazi wengi
- Kuanzisha viwanda hakuhitaji mtaji mkubwa
- Ni rahisi kujaribisha bidhaa katika kiwango kidogo cha kiwanda kidogo
- Viwanda vidogo huchochea usambazaji wa viwanda mashambani
- Hii husababisha ajira kusambazwa nchini
- Usambazaji huleta mweneo wa mapato kote nchini
- Huu ni msingi wa maendeleo
- Viwanda vidogo ni msingi wa kujitegemea kiuchumi

**(b)**

- Tatizo la kwanza ni mtaji.
- Ukosefu wa mikopo ya muda mrefu
- Mikopo ya muda mfupi inatozwa riba kubwa
  - Lipo tatizo kubwa la kawi

- Gharama ya umeme huenda iwe ya juu
- Ukosefu wa maarifa ya kibiashara na ujasiriamali

M a – 8 s – 6 x ½ = 03
b – 5 h – 6 x ½ = 03
ut – 2 z – maneno 10 1z

**MATUMIZI YA LUGHA**

a) Majuso ya majijana yale yalichujuka yalipoanguka (4x ½)

b) Akisoma kwa bidii, atapita mtihani 2x1=02

Akirauka mapema,atapata basi

(lazima pawepo na vitenzi viwili)

c) Abudu-Abudishiana 1x2=02

Mf Wapenzi wale waliabudishiana baada ya kufunga nikahi.

d) "Aisee! Yale mawimbi ya Tsunami (yaliyotokea Bahari HIndi) yaliangamiza biashara nyingi sana." Alisema Bomet. (Vitahiniwa 8x ½ =04)

e) S__S1+U+S2
S1__KN+KT
KN__N
N__Rais
KT__T
T__Alihutubu

U__lakini

S2__KN+KT

KN__O

KT__T

T__Walimpuuza**. 8x ½**

f) Kishazi huru hutoa maana iliyokamilika. Ni sentensi sahihi (alama 3)

Kishazi tegemezinhutoa maana isiyokamilika na hivyo hutegemea kingine kukamilika kimaana

Mf. Ingawa alifunza vizuri,walifeli mtihani.

k.t k.h

g) Ni sentensi agizi (ya masharti) 2x1=02

Au

Ni sentensi ya kuamuru (ya masharti)

h) K.m Kaondokeni (kadiria) 1x1=01

i) (i) chagizo-neno/maneno ambayo huchukua nafasi ya kielezi katika sentensi. (2x1=02)

Kikiondolewa hakiathiri maana ya sentensi

(ii) chagizo- Haraka (1x1=01)

j) Mzee Kambumbu alisema kuwa kile kijicho cha paka cheupe, siku hiyo kingekuwa marufuku kwake. (6x ½ =03)

k) Zawadi(N)- zawidi(T)

k.m Alizawidiwa kwa kupasi mtihani (1x2=02)

l) Jino Ngeli ya LI-YA (4x ½ )

i. Jitu-ukubwa/uduni wa kitu
ii. Kujilia-kirejeshi/kujirejelea
iii. Mkimbiaji-mazoea/uzoefu

m) Ilimradi-ili,iwapo,kwa masharti kwamba,mradi. (Alama 1x2=02)

Mf. Nitaruka maji ilimradi nipewe zawadi

n) Kihisishi cha bezo k.m mmm! Po! Nyoo! Mnh! Ngoo! Mawe! Ebo! Wapi! Zii! Aka! 1x1=01

o) Wa- nafsi (alama 4x ½ =02)

li-wakati uliopita

an-kauli ya kutendana

a-tamati

p) Kiimbo-ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji (alama 1x1=01)

Ni kiwango cha utoaji wa sauti kutegemea ujuu na uchini wake unaowezesha kupata tofauti za hisia za msemaji

q) (i) Vokali- ni sauti zinazotamkwa hewa inapotolewa bila kikwazo/kuzuiliwa (alama 1x1=01)

(ii) /i/ ni sauti ya mbele ya kinywa (alama 2x 1 =02)

Ni sauti ya juu ya kinywa

Midomo hutandazika inapotamkwa

r) Kugawika kwa njia (Alama 2x1=02)

Ingia katika chombo cha kusafiria

Paji la uso

Pembe kubwa inayopigwa nchani

Manati/chombo cha kurushia mawe

**ISIMUJAMII**

a)

- Kiswahili ni lugha ya Kibantu - Lugha ya Kiswahili ina maneno mengi ya Kibantu hivyo basi chimbuko lake ni Kibantu.

- Kiswahili imetokana na lugha ya Kiarabu - Lugha hii ina maneno kadha ya Kiarabu. Hii yaonyesha kuwa ni lugha ya Kiarabu.

- Kiswahili ilitokana na mchanganyiko wa lugha ya Kibantu na Kiarabu - Maneno mengi ya Kiswahili yana asili ya aidha Kibantu ama Kiarabu. Hii yaonyesha kuwa lugha hii ni uzawa wa lugha hizi mbili. (Hoja 3 x 2 = 6)

b)

- Uwili lugha- uwezo wa mtu kuzungumza lugha mbili

- Lingua Franka- lugha inayounana na mazingirganisha watu wanaozungunza lugha tofauti

- Misimu- semi za mda zinazotumika na kikundi fulani cha watu na hutoweka kwa baada ya mda.

- Sajili- matumizi ya lugha kulingana na mazingira 4x1=04

- <u>Jinsi ya kusahihisha matumizi ya Lugha</u>

- Ondoa nusu ($^{1}/_{2}$) kwa kila kosa la sarufi (s) litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu alama ($^{1}/_{2}$) kwa kila kosa la tahajia (h) litokeapo mara ya kwanza hadi makosa sita katika swali lote yaani: *(6 x ½ = 03 )*

<u>Jinsi ya kusahihisha Isimu Jamii</u>

- Ondoa nusu (½)alama kwa kila kosa la sarufi (s)litokeapo kwa mara ya kwanza kwa kila kijisehemu lakini isipite nusu ya alama alizopata (si alizotengewa) katika kijisehemu hicho.
- Ondoa nusu (½) alama kwa kila kosa la hijai (h) litokeapo kwa mara ya kwanza hadi makosa sita yaani *(6 x$^{1}/_{2}$ =03)*